

## 22G-Maddutw-Twabiy'iy - Alifaatu-Hayyin-Twahur:

### v. أَلِفَاتُ حَيِّ طَهْرٍ - Alifaatu-Hayyin-Twahur

Ni مَدُّ الطَّبِيعِي (maddutw-twabiy'iy) inayotokana katika kutamkwa baadhi ya الحُرُوفُ الْمُتَقَاتَةُ (Al-Huruwf Al-Mutaqatw-twa'ah)<sup>1</sup> zinazoanzia baadhi ya Suwrah, kwa vile herufi hizo zinatamkwa kama herufi za hijaiyah ح ا يا ط ا ها را . Nazo zimeundwa katika ibara ya حَيِّ طَهْرٍ (hayyun twahur) kwa jina jingine huitwa أَلِفَاتُ حَيِّ طَهْرٍ (Alifaatu hayyin twahur).

Mfano:

Suwrah	Huruwf Al-Mutaqatw-twa'ah	Herufi
Suwrah saba zinazoanzia	حَم	ح
Maryam Yaasiyn	كَهَيْعَصَ يَسَ	ي
Twaaha, An-Naml, Ashu'araa, Al-Qaswasw	طَه طَسَ طَسَمَ	ط
Maryam, Twaaha	كَهَيْعَصَ طَه	ه
Yuwnus, Huwd, Yuwsuf, Ar-Ra'd, Ibraahiym, Al-Hijr	الر	ر

<sup>1</sup> Rejea mlango wa Maddul-Far'iy - Al-Madd Al-Laazim Al-Harfiyy